**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**CHUO CHA UALIMU TABORA**


Anuani ya simu: “T.T.C.”
TABORA
Simu Na:
0262604939/0752416009
Fax: 0262604939
Email: taboratc@moe.go.tz.

Chuo cha Ualimu Tabora,
S.L.P. 320,
TABORA
**TANZANIA**


**Unapojibu tafadhali taja:**

**Kumb.Na.TBR/CCU/JI/VOL II/19** **13.06.2023**

…………………………………………………….
…………………………………………………….
…………………………………………………….
…………………………………………………….

**YAH: KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA MAALUM YA UALIMU WA SEKONDARI/STASHAHADA YA KAWAIDA YA UALIMU WA SEKONDARI ASTASHAHADA YA UALIMU SHULE YA MSINGI CHUO CHA UALIMU TABORA MWAKA 2023/2024**

## 1.0: UTANGULIZI: -

Ninapenda kukuarifu kuwa umechaguliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kujiunga na Mafunzo ya **Stashahada Maalum ya Ualimu wa Sekondari Masomo ya Sayansi katika Fizikia na Hisabati/Fizikia na Kemia/Hisabati na Tehama/Kemia na Baiolojia. Stashahada ya ualimu wa Sekondari Sayansi/Sayansi jamii/Astashahada ya ualimu shule ya msingi/awali/elimu ya michezo/English medium** katika Chuo cha Ualimu Tabora. Chuo kinakupongeza kwa nafasi hii. Tunategemea kuwa utatumia nafasi hii vizuri katika masomo yako. Hivyo, unatakiwa uwe na juhudi na moyo wa kujifunza darasani na nje ya darasa ili uweze kufaulu vizuri mafunzo yako.

## 2.0: MAHALI CHUO KILIPO : -

Chuo kipo Tabora mjini umbali wa kilometa moja **(1)** Magharibi mwa stesheni ya reli na kilometa moja na nusu **(1½)** Mashariki mwa kituo kuu cha mabasi.

## 3.0: TAREHE YA KURIPOTI: -

Unatakiwa kuripoti Chuoni tarehe **17/7/2023 kwa kozi ya Stashahada Maalum ya Ualimu Sekondari wa Masomo ya Sayansi katika Fizikia na Hisabati/Fizikia na Kemia/Hisabati na Tehama/Kemia na Baiolojia. Pamoja**

**na kozi ya Astashahada ya ualimu elimu awali, msingi, elimu kwa michezo na English medium.** Mwisho wa kuripoti kwa wanachuo wa **Stashahada Maalum ya Ualimu wa Masomo ya Sayansi katika Fizikia na Hisabati/Fizikia na Kemia/Hisabati na Tehama/Kemia na Baiolojia pamoja na astashahada elimu msingi, awali, elimu kwa michezo na English medium** ni tarehe **31/7/2023**

**Wanachuo waliochaguliwa kwa kozi ya Stashahada ya Ualimu wa Sekondari Sayansi/Sayansi jamii wanatakiwa kuripoti tarehe 14/8/2023** ili kuanza mafunzo.
Mwisho wa kuripoti kwa kwa wanachuo wa **Stashahada ya ualimu wa Sekondari Sayansi/Sayansi jamii** ni tarehe 28/8/2023

**TAHADHARI: Mwanachuo akichelewa, yaani akiripoti wiki mbili (SIKU 14) baada ya tarehe ya kuripoti iliyoainishwa hapo juu hatapokelewa**.

## 3.1: MUDA WA MAFUNZO: -

Muda wa mafunzo kwa kozi ya Stashahada Maalum ya Ualimu Sekondari wa Masomo ya Sayansi katika Fizikia na Hisabati/Fizikia na Kemia/Hisabati na Tehama/Kemia na Baiolojia ni **miaka mitatu**. Kwa kozi ya Astashahada ya ualimu elimu awali, msingi, elimu kwa michezo na English medium pamoja na Stashahada ya ualimu wa Sekondari Sayansi/Sayansi jamii ni **miaka miwili**.

## 4.0: USAJILI: -

- Mwanachuo akifika chuoni, lazima aripoti kwa Msajili wa chuo, ili apewe utaratibu wa nini cha kufanya ili kukamilisha usajili wake.

## 5.0: VYETI HALISI:

- Fika na **CHETI HALISI (Original Certificate)** cha kumaliza Kidato cha NNE NA CHA SITA na Cheti cha Kuzaliwa. Ikiwa cheti cha mwaka husika hakijatoka atatakiwa kuja na result slip ya mwaka husika.
- Uje pia na ***'Leaving Certificate'*** yako ya shule uliyomalizia kidato cha Nne na cha Sita isipokuwa kama ulikua mtahiniwa wa kujitegemea (private candidate)
- USIPOKUJA NA VYETI TAJWA HAPO JUU, HUTAPOKELEWA CHUONI. **Tafadhali zingatia sana suala hili.**
- Kama wewe ni Mfanyakazi (mwajiriwa) njoo na **kitambulisho** chako halisi cha kazi na **barua ya ruhusa** kutoka kwa mwajiri wako.
- Kila mwanachuo anatakiwa kuja na kadi yake ya **bima ya afya** kama hana atatakiwa kulipia shilingi **50,400/=** kwa ajili ya kupata kadi y**a bima ya afya** kwa wanafunzi, kwa taratibu za bima ya afya. **Bima ni lazima kwa kila mwanachuo.**

- Hati ya uthibitisho wa Daktari (imeambatatanishwa). Kila mwanachuo anatakiwa kupima katika hospitali za Serikali zinazotambulika na kupigwa muhuri. Kwa wanachuo wenye changamoto kubwa ya afya tunashauri mara afikapo chuoni kuwa wazi kwa walezi na kuwa na uthibitisho wa daktari juu ya tatizo alilonalo sambamba na kuhakikisha dawa zake muhimu anazotumia kufahamika kwa mlezi wa wanachuo au muuguzi wa chuo.

## 6.0: ADA YA CHUO:

- Fedha ya **Ada** ya Chuo ni Tshs. **450,000/=** kwa mwaka. Ada hii inaweza kulipwa kwa awamu mbili yaani Tshs. **225,000/=** kwa muhula au unaweza kulipa kiasi chote Tshs. **450,000/=** kwa mara moja kwa mwaka**.**
- **Ada** hii ya Chuo ilipwe kwa kupewa "control number" na Muhasibu wa Chuo mara ufikapo chuoni au kufanya mawasiliano na uongozi wa chuo mapema ili kutumiwa kwa ajili ya kufanya malipo

## 7.0: MICHANGO MINGINE YA CHUO:

| S/N | MCHANGO | KIASI | MAONI |
|---|---|---|---|
| 1 | Serikali ya wanachuo | 5,000/= | Mwaka |
| 2 | Huduma ya kwanza | 10,000/= | Mwaka |
| 3 | Usafi na mazingira | 20,000/= | Mwaka |
| 4 | Kukodisha godoro | 10,000/= | Mwaka |
| 5 | Usajili na kitambulisho | 20,000/= | Miaka miwili |
| 6 | Michezo | 30,000/= | Mwaka |
| 7 | Ulinzi | 30,000/= | Mwaka |
| 8 | Ukarabati | 25,000/= | Mwaka |
| 9. | BIMA ya Afya | 50,400/= | Mwaka |
| 10 | Mahafali | 10,000/= | Mwaka |
| 11. | T-Shirt | 15,000/= | Mwaka |
| | **JUMLA** | **225,400/=** | |

**Mwanachuo afikapo mwaka wa pili atapaswa kulipia joho la mahafali kiasi cha Tsh 10,000**

**ZINGATIA:**
Michango hii yote ambayo imeorodheshwa hapo juu ilipwe kwenye akaunti ya michango ya Chuo **Na: 51001100030 [NMB]** tawi la **Mihayo Tabora.** Jina la akaunti ni **'*The Principal Tabora Teachers' College'*. Unapofanya malipo, andika aina ya michango uliyolipia kwenye stakabadhi ya malipo ya benki pamoja na jina la mwanachuo husika (Siyo jina la mzazi).**

**MUHIMU SANA**:
Mwanachuo anapolipa ada au michango ya chuo aje na '**Pay in Slip' halisi** au Stakabadhi inayotolewa na Benki husika. Unatakiwa uje na *Stakabadhi/Pay in Slip* mbili, moja inayoonyesha malipo ya ada ya chuo (ikiwa ulishafanya malipo kwa control number) na nyingine ionyeshe michango mingine ya chuo. Ukichanganya malipo hayo hutarudishiwa fedha yako na itakubidi ulipe mara mbili (fanya malipo sahihi kwenye akaunti husika). Vilevile, stakabadhi za malipo zioneshe **jina kamili la mwanachuo** husika na **sio** jina la **mzazi/mlezi** wa mwanachuo.

## 8.0 VIFAA VINGINE KWA AJILI YA MATUMIZI YA CHUO:

Kila mmoja aje na rimu mbili ya karatasi aina ya 'MULTIFUNCTIONAL copy fax inkjet laser prints NO. 1. yenye kava la rangi nyekundu na njano' ambayo atakabidhi ofisi ya Uadili.

### 8.1: Vifaa vya Malazi

- Blanketi **1.**
- Shuka jozi **2 za rangi ya bluu** na mto wenye **foronya ya** bluu.

### 8.2: Vifaa vya Michezo

**WANAWAKE**

- Jezi moja ya taifa stars ya bluu – Inapatikana duka la chuo
- Sketi nyeusi fupi ya kuvaa juu ya suruali
- Track suit ya bluu ya rangi ya bendera Taifa- Inapatikana duka la chuo
- Raba nyeupe na soksi zenye ufito kwa juu

**WANAUME**

- Jezi moja ya taifa stars ya bluu- Inapatikana duka la chuo
- Track suit ya bluu ya rangi ya bendera ya Taifa - Inapatikana duka la chuo
- Raba nyeupe na soksi zenye ufito kwa juu

### 8.3: Vifaa vya Chakula

- Sahani
- Bakuli
- Kikombe (mug)
- Kijiko
- Dumu la lita tano (5) kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kunywa

### 8.4: Vifaa vya Usafi binafsi

- Ndoo ya lita 20
- Kandambili
- Vifaa vya kuwekea sabuni na brash
- Pamoja na vifaa vingine vinavyofaa kwa ajili ya usafi binafsi

### 8.5: Vifaa vya Masomo

- Daftari 12. (Counterbook quire four)

- Kila mwanafunzi aje na spring faili kumi.
- Scientific Calculator (Kwa masomo ya Sayansi), mathematical set, penseli, kalamu za bluu au nyeusi

**N, B: Vifaa vilivyoainishwa hapo juu vinapatikana katika duka la chuo isipokuwa scientific calculator**

- Vifaa vya TEHAMA kama vile flash, laptop vinaruhusiwa. Smart phone itatumika eneo la bweni tu na mwanachuo hataruhusiwa kutumia nje ya hapo. Dhamana ya usalama wa simu ya mkononi ni ya mwanachuo mwenyewe.
- Koti jeupe la kutumia maabara(Kwa wanachuo wanaosoma masomo ya Sayansi tu)

**8.6: Vitabu**

- Kila mwanachuo anatakiwa kuja na **mihtasari** miwili ya masomo yake ya kufundishia, kiongozi cha mwalimu na vitabu vya kiada viwili kwa masomo yake.
  Wanachuo wa Astashahada ya Elimu msingi waje na vitabu vya shule ya msingi kwa darasa la kwanza hadi la saba, wanachuo wa elimu awali waje vitabu vya elimu awali, wanachuo wa English Medium waje na vitabu vinavyotumika kufundishia shule za English Medium. Wanachuo wa Stashahada ya Sekondari waje na vitabu vya kufundishia shule za Sekondati kidato cha kwanza hadi cha nne kulingana na Tahasusi anayochukua.
- Kwa wanachuo wa Stashahada maalum ya Sekondari waje na vitabu vifuatavyo: (Kulingana na masomo anayasoma)

**PHYSICS**

1. Mehta V.K & Mehta R.(2008) *Principals of Physics Class Xi*; S. Chand & Company PVT. Ltd New Delh India
2. Mehta V.K & Mehta R.(2008) *Principals of Physics Class Xii*; S. Chand & Company PVT. Ltd New Delh India
3. Nelkon M. & Parker R (2004) *Advanced Level Physics 7$^{th}$ Ed*; Heinamann Educational Books. London
4. TIE (2020) *Advanced Level Physics Form five*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam
5. TIE (2020) *Advanced Level Physics Form Six*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam

**CHEMISTRY**

1. Jain S.K (2008) *Conceptual Chemistry Class Xi*; S. Chan & Company PVTLtd New Delh India
2. Jain S.K (2008) *Conceptual Chemistry Class Xii*; S. Chan & Company PVTLtd New Delh India

3. TIE (2020) *Advanced Level General Cemistry Form five & Six*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam
4. TIE (2020) *Advanced Level Physical Chemistry Form Five & Six*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam
5. TIE (2020) *Advanced Level Organic Chemistry Form five & Six*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam
6. TIE (2020) *Advanced Level Inorganic Chemistry Form Five & Six*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam

**BIOLOGY**

1. Tylor D.J etal (1997) *Biological Science 3rd Ed*; Amazon Publishers, New York
2. TIE (2020) *Advanced Level Biology Form five*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam
3. TIE (2020) *Advanced Level Biology Form Six*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam
4. Toole G. & Toole S. (2014) New Understanding Biology 4th Ed: Oxiford University Press. London United kingdom

**ADVANCED MATHEMATICS**

1. Backhouse J.K & Houldsworth S.P.T (1985). *Pure mathematics 1 3rd Ed*; Longman Publishers. London
2. Backhouse J.K & Houldsworth S.P.T (1985). *Pure mathematics 2 3rd Ed*; Longman Publishers. London
3. Sadler A.J (1967) *Understnding Pure Mathematics*; Oxford University Press, London United Kingdom

## 9.0 SARE YA CHUO: -

### A. WANAWAKE:

- Sketi 2 dark blue zenye rinda moja tu, shati 2 light blue mikono mirefu na tai 2 ndefu za rangi ya dark blue, Viatu vyeusi vya kutumbukiza visivyo na urembo wowote vyenye visigino vifupi jozi 2 na soksi nyeupe ndefu za kufika juu karibu na goti jozi 2.
- Koti lenye rangi ya dark blue inayofanana na sketi.


**MUHIMU: Sketi iwe ndefu hadi usawa wa kifundo cha mguu. Wanachuo wa dini ya kiislam waje na juba mbili nyeupe zisizofika kwenye viwiko vya mikono.**

**Sare za Ibada kwa wanachuo wa Kiislamu ni Baibui Nyeusi na mtandio Mweupe. Sare hizi zitatumika wakati wa kwenda kwenye Ibada.**


**B. WANAUME:**

- Suruali 2 dark blue zenye marinda na mkanda mweusi, Shati 2 light blue mikono mirefu na tai 2 ndefu rangi dark blue, viatu vyeusi vyenye kamba vya kutumbukiza jozi 2 na soksi nyeusi jozi 2 pamoja na koti lenye rangi ya dark Blue inayofanana na suruali na lenye mipasuo miwili nyuma.
- **Kwa wanachuo wa dini ya Kiislamu vazi la Ibada itakuwa kanzu nyeupe na kofia yake na koti jeusi.**
- **NB: Sare zote zinatakiwa kuwa na mshono ulioainishwa hapo chini katika picha namba 1 na namba 2 kwa wavulana na wasichana. Ikiwa kuna mkanganyiko wa kutambua rangi halisi inashauriwa mwanachuo kushona sare mara afikapo chuoni baada ya kuona rangi halisi inayotakiwa.**

**PICHA Na. 1**



**PICHA Na. 2**



**T-shirt (Wanawake na wanaume) inayovaliwa mwisho wa juma na anapotoka nje ya chuo zinapatikana chuoni kwa Tsh 15,000/= fedha ambayo itatakiwa kulipwa kwenye akaunti ya michango.**

## 10.0 USAFIRI

Unatakiwa ujigharimie mwenyewe kwa nauli ya kuja chuoni na kurudi nyumbani wakati wa likizo.

## 11.0 CHAKULA

Chuo kinatoa chakula kufuatana na uwezo wa serikali.

Chuo hakiruhusu wanachuo kujipikia mabwenini au mahali popote katika eneo la chuo. Hivyo usije na vifaa vya aina yeyote kwa ajili ya kupikia.

Chuo hakina chakula maalum **(special diet)** kwa wenye matatizo ya afya au wenye afya dhaifu ya kudumu.

**12.0 MAWASILIANO:**

Mawasiliano yoyote yanayomhusu mwanachuo kutoka kwa ndugu zake au nyumbani **LAZIMA** yapitie kwenye uongozi wa Chuo, kwa Namba

**026 2604939 – Ofisi ya Mkuu wa Chuo**
**0752416009 – Mkuu wa Chuo**
**0767908900 – Makamu Mkuu wa Chuo**
**0789714356 – Msajili wa Wanachuo**
**0784505465 – Mwadili wa Wanachuo**
**0755679493 – Muhasibu wa Chuo (Kwa masuala ya malipo tu)**

**13.0 NIDHAMU**

Kwa wakati wowote unapokuwa hapa chuoni unatakiwa kufanya mambo sahihi kwa wakati sahihi, mahali sahihi, na njia iliyo sahihi kwa mujibu wa maelekezo ya **KANUNI/NGUZO** za chuo ambazo utazipata mara utakapofika Chuoni.

**14.0 MWISHO**

Kila siku unategemewa kuwa mfano mzuri wa kuigwa kwa kutekeleza **"MOTTO"** wa Chuo ambao ni **"TAA BORA – ANGAZA DAIMA".**

**KARIBU CHUO CHA UALIMU TABORA**

..................................
**Balbina L. Joseph**
**MKUU WA CHUO**

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU TABORA
S.L.P 320, TABORA

**Nakala:** Mkurugenzi Msaidizi Mafunzo ya Ualimu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P. 10,
**40479 DODOMA.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY**
**TABORA TEACHERS' COLLEGE**

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

DATE…………………………………………………………….
Mr/Mrs/Miss……………………………………………………… **(NAME IN FULL)**

Please examine the above named as to **HIS/HER** physical and mental fitness for a full time Teacher Training Course. The Examination should include the following categories.

1 Eye sight
2 Hearing
3 Limbs
4 Speech
5 Veneral deseases
6 Leprosy
7 Epilepsisy
8 Neorosis
9 Other serious deseases
10 Pregnancy

---

## MEDICAL CRTIFICATE

(To be compeleted by Government medical officer)

I have examined the above named and consider that **HE/SHE** is physically **FIT/UNFIT** and mentally **FIT/UNFIT** to full time Teacher Training Course.

1 Eye sight……………………………………………………………………
2 Hearing…………………………………………………………………..
3 Limbs……………………………………………………………………
4 Speech……………………………………………………………………
5 Veneral deseases…………………………………………………………
6 Leprosy…………………………………………………………………..
7 Epilepsisy………………………………………………………………..
8 Neorosis………………………………………………………………….
9 Other serious deseases……………………………………………………
10 Pregnancy ……………………………………………………………….

**Approved by :**

**Name……………………………Signature…………………. Date…………………….**